## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

**Kumb.Na. MM/AR/S.20/12/VOL IV/9** **26 Mei, 2025**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha anawatangazia wananchi wote ambao ni Raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapa chini:-

### 1.0 MWANDISHI WA HABARI NA MTANGAZAJI WA REDIO DARAJA LA II – (NAFASI I)

### 1.1 MAJUKUMU YA MWANDISHI WA HABARI NA MTANGAZAJI WA REDIO DARAJA LA II

i. Kuandaa na kuvirusha vipindi vya Radio

ii. Kutafuta na kukusanya taarifa za Radio.

iii. Kuaanda Makala maalum ya Radio kuhusu matukio mbalimbali yanayotokea nchini na nje ya nchi.

iv. Kuhariri vipindi vya Radio.

#### 1.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe na shahada au Stashahada ya juu ya Uandishi wa Habari au Fani ya 'Mass communication kutoka chuo kinachotambuliwa na Serekali.

#### 1.1.2 MSHAHARA

Mshahara utakuwa Tshs.500,000/-

### 1.2 MWANDISHI WA HABARI NA MTANGAZAJI MSAIDIZI (NAFASI 3)

#### 1.2.1 MAJUKUMU YA MTANGAZAJI MSAIDIZI

i. Kukusanya na kuandika habari za matukio mbalimbali katika jamii.

ii. Kuendesha vipindi mbalimbali vya Radio.

iii. Kuandaa vipindi vya Radio.

### 1.2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe mwenye cheti cha mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV ambao wamehitimu mafunzo ya miaka miwili katika fani ya Uandishi wa Habari katika chuo kinachotambulia na serikali.

**MSHAHARA**

Mshahara utakuwa Tshs.300,000/-

### 1.2.3 AFISA MASOKO (NAFASI 1)

### 1.2.4 MAJUKUMU YA AFISA MASOKO

(i) Kufanya tafiti za masoko, kukuza na kutekeleza mipango ya masoko ya Radio Enaboishu FM.

(ii) Kutangaza huduma zitolewazo na kituo cha Radio Enaboishu FM.

(iii) Kuandaa mikakati mbalimbali ya (Kampeni) kupata matangazo kwa ajili ya kituo cha Radio Enaboishu FM.

(iv) Kutafuta wadau/wateja kwa ajili ya kutangaza huduma zao kupitia kituo cha Radio Enaboishu FM.

(v) Kutoa taarifa ya kila mwezi ya utekelezaji wa masoko kwa Mkurugenzi.

(vi) Kusimamia shughuli zote za matangazo ya vipindi vya Radio Enaboishu FM.

### 1.2.5 SIFA ZA MWOMBAJI

(i) Awe na Elimu ya Diploma ya Biashara kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.

(ii) Awe na uwezo wa kuzungumza lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha.

(iii) Awe amesomea kompyuta angalau mwaka mmoja.

(iv) Awe mwenye kujiamini na mwenye uwezo wa kumshawishi mteja.

(v) Awe na miaka kati ya 25-45

(vi) Awe mzoefu katika kazi hii upande wa Radio usiyopungua miaka 2.

**MSHAHARA**

Mshahara utakuwa Tshs.400,000/-

## 1.6 MASHARTI YA JUMLA

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko ajiriwa Serikalini.

ii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza

iii. (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/ Diploma/Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Computer Certificate.**

v. "Testmonial", "Provisional Results", "Statement of results", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

vi. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE**).

vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

viii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **08 Juni, 2025**.

ix. Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA,**
**S.L.P. 2330,**
**ARUSHA**

x. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATASHUGHULIKIWA**

Tangazo hili limetolewa na:-

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA
ARUSHA

Seleman H. Msumi
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**